JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA
SHULE YA SEKONDARI YA NASIBUGANI
"Barua zote zielekezwe kwa Mkuu Wa Shule"

Simu:

Mkuu wa Shule,
Shule ya sekondari Nasibugani,
S.L.P 6,
Mkuranga.

Kumb Na. NSSF/FISEC/VOL.1/2018/…..

Tarehe……/……/20……

Mzazi / Mlezi wa…….
S. L. P……
……...

YAH: TAARIFA YA MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018/2019 SHULE YA SEKONDARI NASIBUGANI

1.0 UTANGULIZI

Bodi ya shule, walimu, wafanyakazi na wanafunzi wa shule ya sekondari Nasibugani wanakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka 2018 na wanakukaribisha katika shule hii. Ni imani yetu utaitumia nafasi hii adimu kusoma na kujifunza kwa bidii na uwezo wako wote pamoja na kushirikiana na wenzako, walimu na jumuiya nzima ya Nasibugani ili kulinda heshima na sifa ya shule kwa maendeleo ya Taifa letu.

2.0 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Nasibugani ipo katika kijiji cha Nasibugani, kata ya Msonga, tarafa ya Kisiju, Wilaya ya Mkuranga mkoa wa Pwani. Umbali wake ni km 48 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Mkuranga upande wa mashariki jirani na bahari ya Hindi. Usafiri wa mabasi unaanzia Mbagala rangi tatu DSM kupitia barabara kuu iendayo mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara hadi kijiji cha Nyamalonda na kufika eneo la Msonga. Pia usafiri unapatikana eneo la mbagala rangi3 kuelekea Kisiju Pwani na baada ya kufika kituo cha Mavunja unakunja upande wa kulia. Shule itafunguliwa kwa mujibu wa tangazo la serikali, kwahiyo kila mwanafunzi anapaswa kufuatilia matangazo ya serikali.

3.0 KICHOKOO CHA SHULE "SCHOOL MOTTO"

Kichokoo cha shule (school motto") ni tamko rasmi linaloelekeza au kutoa mwelekeo wa shule. Kichokoo cha shule ya sekondari Nasibugani ni **"ELIMU NI UKOMBOZI" (EDUCATION IS FOR LIBERAATION)**. Ukiwa mwanafunzi wa shule hii tunatarajia utakuwa na nidhamu ya hali ya juu itakayokuwezesha kujijenga kitaaluma na ufanisi mkubwa na hivyo kwa kujikomboa kimaisha na kuwa mtaalamu / raia mwema wa Taifa la kesho.

4.0 MAHITAJI YA SHULE
A. SARE ZA SHULE

WAVULANA

i. Suruali dark blue mbili (zenye marinda mawili mbele kila upande) na tai moja utashonewa hapahapa shuleni kwa Tshs 45,000/= (utatoa fedha taslimu kwa mhasibu siku hiyo hiyo)
ii. Shati mbili nyeupe zenye mikoni mirefu (Aje nazo mwanafunzi mwenyewe)
iii. Mwanafunzi aje na suruali za kaki mbili akiwa ameivaa. Suruali za kaki za kitambaa zenye marinda mbele, atakuwa anavaa suruali hizo siku ya Jumamosi, Jumapili na siku ambazo hakuna masomo.
iv. Fulana (Tshirt) yenye kola na nembo ya shule inapatikana shuleni kwa Tshs 15,000/= utatoa fedha taslimu siku hiyo hiyo)
v. Mkanda mweuzi, viatu vyeusi vyenye visigino vifupi (gidamu) soksi nyeusi jozi mbili, sweta ya rangi dark blue yenye msuko wa V mbele, nguo za michezo (track suit)
vi. Lazima kuja na chandarua, shuka mbili za light blue, mto, foronya, ndoo ndogo ya lita 10, vyombo vya chakula**(vyombo viwe vya mfupa au udongo na si vya plastic)** na vifaa vingine vya usafi wa mwili. Unaweza kuvinunua Mbagala ili kupunguza usumbufu.
vii. Kila mwanafunzi anapaswa kuja na stempu tatu kwa ajili ya kutumia matokeo yake (Kila stemp iwe na thamani ya kutumia barua moja ya kawaida).

5.0 MAHITAJI MENGINE MUHIMU SANA

NA	MAELEZO	KIASI
i.	Ada	70,000
ii.	Taaluma	40000
iii.	Mchango huduma ya kwanza NHF na dawa baridi	20,000 (ilipwe yote mara moja)
iv.	Ulinzi na mpishi	20,000/=
v.	Tahadhari (isiyorudishwa)	10,000 kwa miaka miwili
vi.	Dawati	15000/= kwa miaka miwili
vii.	Kitambulisho na usajili	20,000/= kwa miaka miwili
viii.	Ukarabati	25,000/=
ix.	Umeme na maji	20,000/=
x.	Mahafali	10,000/=
xi.	Godoro*	25,000/=
xii.	Skauti na mazingira	25,000/=
xiii.	Elimu ya vitendo kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi. (CBG)	20,000/=
	Jumla	**320,000/=**

Tanbihi
Fedha yote ilipwe **NMB A/C NO. 20701200159** jina la akaunti SHULE YA SEKONDARI NASIBUGANI. Hatupokei fedha taslimu katika kipengele nambari (i – xiii)

6.0 VIFAA VYA DARASANI

a) Daftari kubwa ‘counter book za kutosha
b) Mkebe wa hisabati na kikokotozi kwa tahasusi ya CBG
c) Advanced learners dictionary moja, rula yenye cm 30, kalamu za wino na penseli za kutosha.
d) Bunda la karatasi (ream A4) moja kwa mwaka.

7.0 VIFAA VYA KAZI

i. Kwanja moja kwa wanafunzi wa CBG
ii. Jembe lenye mpini kwa wanafunzi wa HGL

MWISHO

a) Zingatia tarehe ya kufungua shule ili kuleta ufanisi kwenye kalenda ya masomo
b) Simu pamoja na nguo za nyumbani haziruhusiwi. Kabla ya kuruhusiwa kuingia bwenini utapekuliwa
c) Unatakiwa kuja na "Result slip" yako ya kidato cha nne na cheti cha kuzaliwa
d) Mwanafunzi aje shule akiwa amevaa suruali ya kaki na Tshirt nyeupe (mikono mifupi) au fulana isiyo na maandishi na si vinginevyo.
e) Hakikisha una pima afya yako kwenye hospitali inayotambulika na serikali.
f) Kwa mawasiliano piga simu

0787 442 428/0711455209 - Mkuu wa Shule
0717 487 411 – Makamu Mkuu wa Shule
0658 735 420 - Taaluma

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NASIBUGANI

……..
MZEE LWIMBO
MKUU WA SHULE

***Mwanafunzi anaruhusiwa kuja na godoro lake, ambalo halitokuwa na kunguni wala chawa. Iwapo utatumia godoro la shule utapaswa kulipia Tsh 25,000/- na atawajibika kulitunza na kulikabidhi likiwa katika hali nzuri, pindi amalizapo masomo yako.**